# WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA



**Jarida la Mtandaoni**

Limeandaliwa na;
**Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara** | **www.mit.go.tz**

viwandabiashara

# MAJALIWA: UJENZI WA KIWANDA CHA MBOLEA CHA ITRACOM NI SAHIHI





WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema maamuzi yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kumkaribisha muwekezaji wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea cha Itracom ni sahihi kwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Amesema Serikali itasimamia ujenzi wa mradi huo ili kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais Samia ya kuendeleza sekta ya kilimo inafikiwa kwa sababu changamoto kubwa iliyokuwa inawakabili wakulima wengi ni upatikanaji wa mbolea ambayo inakwenda kuwa historia.

Waziri Mkuu ameyasema hayo leo (Jumamosi, Januari 15, 2022) wakati akizungumza na uongozi na wafanyakazi wanaojenga kiwanda hicho katika eneo la Nala jijini Dodoma. "Serikali imedhamiria kuimarisha sekta ya kilimo ili Watanzania wanaoitegemea wapate mafanikio."

Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye leo alifanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo amesema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wake na kwamba Serikali inataka kuona Watanzania wengi wananufaika na uwekezaji huo. Ujenzi wa kiwanda hicho umefikia asilimia 52.

**"Ujenzi wa kiwanda hiki ni matokeo ya ziara ya Mheshimiwa Rais Samia nchini Burundi, lengo ni kuhakikisha tunazalisha mbolea hapa nchini badala ya kutegemea kuagiza nje kwa kiasi kikubwa, kiwanda hiki kinatarajiwa kuzalisha tani 600,000 kwa mwaka".**



Wakati huo huo, Mheshimiwa Majaliwa ametumia fursa hiyo kuwaagiza wataalamu wa Wizara wa Kilimo wahakikishe mbolea itakayozalishwa kiwandani hapo inakwenda sambamba na mahitaji halisi ya wakulima nchini kutokana na aina ya udongo wa maeneo husika.



Pia, Mheshimiwa Majaliwa amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Anthony Mtaka ahakikishe barabara inayokwenda kiwandani hapo inakarabatiwa ili iweze kupitika vizuri katika kipindi chote cha mwaka na kurahisisha usafirishaji wa mizigo mbalimbali ikiwemo mitambo.

Kwa upande wake, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe amesema Wizara ya Kilimo itatoa ushirikiano wa kutosha kwa muwekezaji huyo. Amesema mahitaji ya mbolea kwa sasa nchini ni wastani wa tani 700,000 kwa mwaka, hivyo Ujenzi utasaidia kuondokana na upungufu wa kuagiza mbolea nje ya Nchi. Tanzania inatumia dola milioni 450 kuagiza mbolea nje.



Naye, Naibu Waziri wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe amesema wizara yao inatambua uwekezaji mkubwa uliofanyika katika eneo hilo ambao pamoja na mambo mengine unakwenda kulisaidia Taifa katika kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza mbolea nje ya nchi.

# SERIKALI HAITAVUMILIA WAFANYABIASHARA WANAOPANDISHA BEI ZA BIDHAA KIHOLELA

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji amesema Serikali haitavumilia tabia ya wafanyabiashara wachache wenye dhamira ovu ya kuwaumiza wananchi kwa kujiamulia kupandisha bei za bidhaa bila kufuata utaratibu kwa manufaa yao binafsi kwa kuwa Serikali inajukumu la msingi la kusimamia ushindani wa haki kwenye soko kwa kudhibiti mienendo hadaifu au kandamizi ya wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara wanaopandisha holela bei za bidhaa nchini.

Waziri Kijaji ameyasema hayo alipokuwa akitoa taarifa ya uchunguzi uliotokana na Tume ya Ushindani Tanzania (FCC), kuhusu uhaba na kupanda kwa bei za vinywaji baridi uliotokea mwezi Oktoba, 2022 hadi Januari, 2022 uliotokana na kutopatikana kwa sukari ya viwandani sababu ya ukosefu wa Makasha ya kusafirishia shehena ya sukari hiyo kuja hapa nchini uliojitokeza duniani kote kutokana na athari za UVICO-19, kwa Waandishi wa Habari mara baada ya kutembelea kiwanda cha Jambo Food Products kilichopo Mkoa wa Shinyanga Januari 23, 2022kuangalia hali ya uzalishaji wa bidhaa za mbalimbali hususani vinywaji baridi.





Aidha Waziri kijaji aliwahakikishia watanzania kuwa Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa Sukari hiyo ya viwandani inapatikana kwani hadi sasa tani 25,000 ya sukari ya viwandani imeingia nchini kupitia bandari ya Dar es salaam na inaendelea kupokelewa kwa kuwa Sukari hiyo kwa sasa inasafirishwa kwa njia mbadala ya ufungashaji shehena usiotumia makasha (containers), yaani break-bulk.

Akielezea hatua nyingine ambazo Serikali imechukua ili kutatua changamoto hiyo, Waziri Kijaji amezielekeza Mamlaka na Taasisi za Serikali zikiongozwa na Tume ya Ushindahi (FCC) zilizopewa dhamana ya kusimamia mienendo ya masoko ya bidhaa kutekeleza wajibu huo kikamilifu na kwa umakini mkubwa ili kudhibiti mienendo hadaifu au kandamizi ya wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara kwenye soko ikiwa ni pamoja na upandishaji holela wa bei za bidhaa nchini.

Aidha, Waziri Kijaji amewaelekeza Maafisa Biashara wa Mikoa kote nchini kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye maeneo yao na kuwasilisha taarifa hizo mara kwa mara Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, ili itakapobidi hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati kwa kuwa licha ya kuadimika kwa Sukari ya viwandani, wazalishaji wa vinywaji baridi hawakupandisha bei, isipokuwa mawakala wa usambazaji na wafanyabiashara ndiyo waliopandisha bei, na kuonya tabia hiyo isijirudie tena na watakaobainika watachukuliwa hatua.

Pia Waziri Kijaji amewahakikishia Watanzania kuwa Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuongeza ufanisi katika uondoshaji wa shehena bandarini, kuboresha usafirishaji kwenye barabara kuu na kuimarisha upitishaji wa mizigo mipakani kwa kuwa imeanzisha mfumo wa utoaji wa vibali vya kuagiza sukari ya viwandani kwa njia ya mtandao ili vibali hivyo vipatikane kwa wakati na bila usumbufu wowote na kuhakikisha wazalishaji hawaishiwi malighafi hiyo muhimu ili kuondokana na changamoto ya uingizaji sukari ya viwandani hiyo.

Dkt Kijaji pia amesema Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na kuwekeza nchini kwa lengo la kujenga uchumi imara wa viwanda ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa sukari ya viwandani hapa nchini ili kuondoa utegemezi wa kuagiza sukari hiyo kutoka nje.

**“Natoa wito kwa wawekezaji kuja hapa nchini kuwekeza viwanda vya Sukari ya viwandani, sababu kuna maeneo mengi yametengwa kwa ajili ya uwekezaji, hali ambayo itasaidia kutotokea tena tatizo la kuadimika kwa Sukari hiyo, sababu itakuwa ikizalishwa hapa nchini na siyo kuagiza nje ya nchi.”**

Awali kabla ya ziara katika kiwanda hicho akiwa ameambatana na viongozi mbalimbali wa Serikali akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Sophia Mjema na Mkuu wa wilaya ya Shinyanga Mhe. Jasinta Mboneko pamoja na baadhi ya wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama Mkoa, Waziri kijaji alitembelea ofisi ya mkuu wa mkoa wa Shinyanga Bi Sophia Mjema na kupata taarifa ya maendeleo ya sekta ya Uwekezaji Viwanda na Biashara pamoja na changamoto mbalimbali ambazo amesema kuwa Serikali itaendelea kuzishughulikia ili kuweka mazingira bora ya uwekezaji na ufanyaji Biashara katika mkoa





# DKT. KIJAJI: TANZANIA INATAKA KUONA MKATABA WA AfCFTA UNAKUWA CHACHU YA KUONGEZA FURSA ZA KIBIASHARA NA UWEKEZAJI KWA NCHI ZA AFRIKA.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.) kwa niaba ya Serikali amelithibitishia Baraza la Mawaziri wa Biashara wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) nia ya Tanzania kuona Mkataba wa AfCFTA unakuwa chachu ya kuongeza fursa kwa nchi za Afrika kupanua zaidi biashara baina yao na kukuza uwekezaji kwa ajili ya maendeleo ya Bara la Afrika.

Waziri Kijaji ameyasema hayo alipokuwa akishiriki Mkutano wa Nane wa Baraza la Mawaziri wa Biashara wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika, uliofanyika Accra, Ghana tarehe 28-29 Januari 2022. Waziri Kijaji aliongoza ujumbe wa Tanzania kushiriki katika Mkutano huo.

Mkutano huo unaofuatia hatua muhimu ya Tanzania kuridhia na kujiunga katika Mkataba wa Kuanzisha Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kupitia Azimio la Bunge la Tanzania la Septemba 9, 2021 nakuifanya Tanzania kuwa nchi ya 40 kuridhia na kuwasilisha Hati ya Kuridhia Mkataba huo kwenye Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AUC). Amesema Waziri Kijaji.

Aidha, Mkutano huo uliohudhuriwa na nchi wanachama wa AfCFTA umejadili masuala muhimu yaliyosalia kuridhiwa ili kuwezesha biashara baina ya nchi za Afrika kuanza kufanyika chini ya Mfumo wa Eneo Huru la Biashara Afrika. Masuala hayo muhimu ni pamoja na ufunguaji wa biashara ya bidhaa, ufunguaji wa biashara ya huduma, vigezo vya uasili wa bidhaa, hakimiliki na ubunifu, uwekezaji pamoja na Sera ya Ushindani. Amesema Dkt. Kijaji

Dkt. Kijaji ameeleza kuwa Baraza hilo la Mawaziri limeridhia kwakauli moja mapendekezo ya hatua mbalimbali zilizopendekezwa ili kuharakisha mchakato wa kukamilisha majadiliano katika maeneo hayo yaliyobakia ili kutimiza kiu ya wadau wengi, hususan Sekta Binafsi barani Afrika kufaidika na uanzishwaji wa Eneo hilo lenye walaji takriban bilioni 1.3 linalotarajiwa kuleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi, kibiashara na kijamii barani Afrika.

Wakati huo huo, Akiwa Ghana, Waziri Kijaji amekutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Ghana Mhe. Alan Kyeremanten ambapo wamejadiliana namna ya kuanzisha mahusiano ya kimkakati ya kibiashara kati ya Tanzania na Ghana ili kuhakikisha uhusiano mzuri wa kisiasa na kihistoria uliopo baina ya nchi hizo mbili unakuwa na manufaa ya kiuchumi kwa wananchi wa Tanzania na Ghana.

Aidha, Katika kikao hicho Mawaziri hao walikubaliana pia kuchukua hatua za makusudi kuwaunganisha wadau wa Sekta Binafsi pamoja na wafanyabiashara wa nchi hizo mbili kwa kuanzisha makubaliano rasmi na kuratibu ziara za mara kwa mara za kibiashara na kubadilishana utaalam na uzoefu katika masuala ya biashara na uwekezaji.

Vilevile, Waziri Kijaji alipata fursa ya kukutana na kuzungumza na Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya AfCFTA Mhe. Wamkele Mene, ambapo Katibu Mtendaji huyo alimpongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa sekta muhimu ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara na kuahidi kuendeleza ushirikiano wa Sekretarieti katika kuhakikisha maslahi ya Tanzania yanazingatiwa kikamilifu katika mchakato wa kukamilisha uanzishwaji wa Eneo hilo Huru la Biashara Afrika.



# DKT. KIJAJI - SERIKALI ITAENDELEA KUBORESHA MAZINGIRA YA UWEKEZAJI NA UFANYAJI BIASHARA NCHINI

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt, Ashatu Kijaji, amekutana na wawekezaji, na wamiliki wa viwanda mbalimbali na kujadiiili changamoto wanazokabiliana nazo na kuahidi kuzitafutia ufumbuzi kwa pamoja ili kutimiza lengo la Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini na kujenga uchumi shindani na viwanda.

Katika mikutano hiyo, Waziri Kijaji amekutana na Viongozi wa Kampuni ya Dangote Tanzania inayozalisha Saruji, Kampuni ya Coca - Cola Kwanza ltd inayozalisha bidhaa mbalimbali za vinywaji baridi na Wawekezaji wa Kampuni ya Gynile kutoka Misri inayotarajia kuanzisha kiwanda cha kuzalisha mbolea nchini.

Wakati huo huo, Waziri Kijaji amekutana na baadhi ya Watendaji na Wakuu wa Tume ya Ushindani (FFC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB ) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) zilizo chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kujadili utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ili kuleta maendeleo kwa taifa.

Aidha Waziri Dkt. kijaji amezitaka taasisi zote chini ya Wizara Uwekezaji Viwanda na Biashara kufanya kazi kwa ushirikikiano na kuepuka kuwa kikwazo kwa wawekezaji, wenye viwanda na wafanyabiashara ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini ili kuendeleza na kukuza sekta ya uwekezaji, Viwanda na Biashara.







# KONGANI YA VIWANDA KUJENGWA DODOMA






Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) amesema Serikali imeanzisha Kongani ya Viwanda Dodoma itakayokuwa na viwanda vitakavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika uanzishaji wa kongani za viwanda.

Dkt Kijaji ameyasema hayo katika Hafla fupi ya makabidhiano ya eneo maalum la uwekezaji (SEZ) lenye ukubwa wa hekari 1500 katika eneo la viwanda Nala lililotolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kwa Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji na Mauzo ya Nje (EPZA), iliyofanyika jijini Dodoma Januari 20, 2022.

"Kongani hii itumike kuhudumia Kanda ya kati kwa kuwa na viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo hususan Alizeti inayolimwa Dodoma, Singida na Simiyu ili kuwa na mafuta ya kula ya kutosha mahitaji ya ndani na kuuza nje ya nchi na kutumia Reli ya Kisasa ya SGR kwa kusafirisha mizigo kwenda masoko ya nje ya nchi." Amesema Waziri Kijaji.

Waziri Kijaji pia amezielekeza Taasisi za EPZA na TIC kushirikiana na Sekta Binafsi pamoja na Uongozi wa Mkoa wa Dodoma ili kuhakikisha kongani hiyo inaendelezwa kwa wakati ili kutimiza malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita katika uanzishaji, uendelezaji na uwekezaji wa kongani za viwanda nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Antony Mtaka amebainisha Maeneo ya EPZA yanavutia wawekezaji hivyo Ofisi yake iko tayari kushirikiana na Wizara katika kuhakikisha miundombinu muhimu kama Maji, Umeme na Barabara inapatikana ili kukamilisha ujenzi wa kongani hiyo kwa wakati na kuvutia wawekezaji na hivyo kuleta maendeleo katika mkoa huo na kwa Taifa.

Kwa upande wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Prof.Godius Kahyarara amesema ni muhimu EPZA kutenga maeneo ya kongani za kiuchumi zenye hadhi ya kimataifa kwa kuzingatia wawekezaji wadogo zinazolenga kutoa ajira nyingi ili kutimiza Malengo ya Serikali katika kuongeza ajira na pato la Taifa.

"EPZA tengeni kongani maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya uzalishaji bidhaa za ujenzi ili kutosheleza mahitaji ya vifaa hivyo nchini ili tusiwe tunaagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi.

Awali akiongea, Mkurugenzi Mkuu wa EPZA Bw. Charles Itembe amesema eneo hilo lililotengwa linatarajiwa kuwa kitivo maalumu cha uwekezaji katika nyanja mbali mbali kama vile ununuzi,usafirishaji, kilimo, ujenzi, madinj, nguo na dawa na litatoa ajira takriban 100,000.

Naye, Afisa Mipango Miji wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Aisha Masanja amebainisha kuwa Mkoa umetenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ambapo katika eneo la Nala hekari 2285 ambapo hadi sasa hekari 300 zimegawiwa kwa wawekezaji wa nje, 1500 kwa EPZA, na 21 kwa wawekezaji wazawa.

# WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA ATOA SIKU TATU KWA FCC KUELEZA SABABU ZA KUADIMIKA VINYWAJI BARIDI

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Dkt. Ashatu Kijaji ameitaka Tume ya Ushindani (FCC) kutoa sababu za kuadimika kwa vinywaji baridi sokoni pamoja na kupanda bila utaratibu kwa bei ya vifaa vya ujenzi.

Akizungumza na watumishi wa Wizara hiyo Dkt. Kijaji amesema kwa siku za karibuni kumekuwepo na kuadimika kwa vinywaji baridi hali iliyopandisha bei ya bidhaa hiyo.

"Hivi ni kweli tunasubiri mwezi mzima soda zinapotea na bei zinaanza kupanda ndiyo tunakuja, hii siyo sawa hivyo naomba ndani ya siku tatu nipate taarifa ya kwanini soda zimeadimika ndani ya soko la Taifa letu" Dkt. Kijaji

"Lakini ndani ya siku Saba pia nipate taarifa ya sababu za kupanda kwa bei ya vifaa vya ujenzi ili tuwambie watanzania kuwa bei halisi unayopaswa kununua nondo ni hii na bei halisi unayopaswa kununua saruji ni hii, hatupangi bei maana ni Uchumi wa soko huria lakini tunafanya utafiti kwa manufaa ya wananchi wetu" Dkt. Kijaji

Amesema pia kumekuwepo na ongezeko kubwa la bei ya vifaa vya ujenzi na ikishaongezeka haipungui tena.




Ni wajibu wa Tume ya Ushindani kutuambia nini kimesababisha bei ya vifaa vya ujenzi ipande na sasa bei ya vinywaji baridi nayo imepanda baada ya kuadimika kwa muda, ni lazima FCC mtuambie sababu za kupanda huko.

"Uchumi wa Taifa letu ni soko huria, lakini ni soko huria kwa kiwango kipi? Hivi kweli kilichosababisha saruji ipande ni nini? Hivi kweli ni kwa sababu Serikali ilisema inakwenda kujenga madarasa Elfu 15? Sasa tumeshamaliza kujenga madarasa mbona hatuoni bei zinashuka."

Dkt. Kijaji amesema ni wajibu wa Wizara hiyo kupitia FCC kumlinda mlaji huku akigusia suala la mbegu ambazo wakati mwingine wakulima wanauziwa zikiwa chini ya kiwango na kuwataka wawe na utaratibu wa kufanya tafiti.

Amesema ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni moyo wa Uchumi wa nchi maana kila kitu kinachogusa Uchumi kinauhusiano mkubwa na Uchumi.

"Tukishawekeza, tukazalisha tunawahitaji wafanyabiashara ndani na nje ya nchi yetu ilikuwezesha kilichozalishwa kifike sokoni" Dkt. Ashatu Kijaji

Amesema upo ulazima wa kujua mahitaji ya soko la nje kuwa ni kitu gani kinahitajika ili msukumo uelekezwe kwenye maeneo hayo na kutaka walaji wapatiwe bidhaa bora kulingana na thamani ya fedha zao.

Amesema jukumu la kuhakikisha bidhaa zinazopelekwa kwa walaji kinakidhi ubora kulingana na thamani ya fedha zinazotolewa ni la FCC hivyo wanapaswa kusimamia kikamilifu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa FCC William Erio amesema wamepokea maelekezo ya Waziri na wameanza kuyafanyia kazi ili kuona kama kupanda huko kumetokana na uhalisia wa uzalishaji au kumekiuka kanuni za Ushindani.

# CAMARTEC YAAGIZWA KUBUNI TEKNOLOJIA RAHISI NA NAFUU KWA WAKULIMA



Naibu Waziri wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe (Mb) amekiagiza Kituo cha zana za Kilimo na Teknolojia vijijini (CAMARTEC) kubuni teknolojia zenye tija kwa gharama nafuu na rahisi kulingana na uwezo wa wakulima na wafugaji nchini bila kuathiri ubora wa teknolojia hizo ili kufikia malengo ya Taifa kuwa nchi yenye maendeleo ya kiteknolojia na uchumi wa kati-juu ifikapo mwaka 2025.

Mhe. Exaud Kigahe (Mb) ameyasema hayo wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi ya 11 ya Kituo hicho, chenye lengo la kukuza matumizi ya zana za kilimo na teknolojia sahihi za vijijini ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi vijijini, uliofanyika katika ofisi za CAMARTEC – Arusha.

Akizindua Bodi hiyo, Mhe. Kigahe alisema Bodi hiyo ina jukumu la kuandaa Mipango na Mikakati mipya ya kuendeleza Kituo hicho ili kukiwezesha kutoa mchango wake kwa uhakika katika kutekeleza msimamo na mtazamo wa Serikali katika kuendeleza Viwanda na kukuza uchumi wa nchi kwa kuwezesha upatikanaji wa malighafi zinazotokana na uendelezaji Kilimo.

"Bodi mnalo jukumu kubwa la kutengeneza mkakati wenu wa kuhakikisha kwamba, malengo ya Taasisi yanafikiwa kwa kusimamia utekelezaji wa mipango yote ya Taasisi. Aidha, katika hili Bodi na Menejimenti mtapimwa kupitia Mkataba wa Utendaji Kazi (Performance Contract) ambao mtausaini Wajumbe wa Bodi, kupitia kwa Mwenyekiti wa Bodi, na Msajili wa Hazina." Amesema Mhe. Kigahe.

Aidha, Mhe. Kigahe amesisitiza uwepo wa mahusiano mazuri na yenye tija na ushirikiano kati ya Bodi, Menejimenti na Serikali na kuhakikisha kuwa vyombo vyote vitatu vinafanya kazi kama timu muda wote. Pia aliasa Bodi na menejimenti ya CAMARTEC kufanya uchambuzi wakina kuhusu miradi wanayotaka kuitekeleza kabla ya kuiwasilisha na kuhakikisha usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo.

Pia naibu Waziri na wajumbe wa bodi walipata fursa ya kutembelea karakana za CAMARTEC na kujionea mwenyewe ubunifu wa teknolojia mbalimbali unaofanywa na kuahidi kuwa Wizara itaendelea kushirikiana na Kituo hicho katika kuhakikisha kuwa Vitovu vya Teknolojia za Kihandisi vinaanzishwa kwa wingi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yana uhitaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ambayo ni malighafi muhimu sana ya viwanda vingi nchini vinavyochangia kuongeza wigo wa ajira kwa vijana na akina mama nchini.

Naye, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Viwanda Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara,akimukaribisha Naibu Waziri kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo aliwashauri wajumbe hao kufanya kazi kwa pamoja na Wizara ili kuiwezesha CAMARTEC kusaidia jitihada mbalimbali katika kuboresha mnyororo wa thamani na kuuza mazao yaliyoongezewa Thamani.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya CAMARTEC iliyozinduliwa, Prof. Valerian C. K. Silayo aliahidi kufanya kazi kwa ushirikiano katika kutekeleza maagizo yaliyotolewa na kuifanya CAMARTEC kufikia malengo yaliyokusudiwa katika kusaidia wakulima ili kuongeza uzalishaji katika kilimo na kuboresha hali ya maisha ya wananchi vijijini.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa Kituo kwa Naibu Waziri na wajumbe wa Bodi, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CAMARTEC, Bw. Pythias M. Ntella alisema kwa mujibu wa Sheria CAMARTEC inafanya utafiti unaozingatia mahitaji ya wadau inatoa mafunzo na kuhawilisha zana za kilimo na teknolojia za vijijini na inafanya majaribio na kuthibitisha ubora wa zana za kilimo na teknolojia sahihi za vijijini.









# TANZANIA ITAENDELEA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA KUTEKELEZA MKATABA WA AFCFTA

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Prof. Godius Kahyarara amesema Tanzania itaendelea kushirikiana na Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara Afrika AfCFTA, Sekta Binafsi na Wadau wengine nchini kuwaelimisha wananchi kuchangamkia fursa za biashara na uwekezaji zinazopatikana katika Eneo hilo.

Katibu Mkuu ameyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya AfCFTA Mhe. Wamkele Mene Januari 24, 2022 katika Ofisi za Makao Makuu ya Sekretarieti hiyo yaliyopo Accra, nchini Ghana.

Pamoja na mambo mengine yaliyojiri katika mazungumzo hayo, Prof. Kahyarara alimpongeza Mhe. Wamkele kwa hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mkataba wa AfCFTA na kusisitiza utayari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kushiriki kikamilifu katika kutekeleza Mkataba huo.

Naye Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya AfCFTA Mhe. Wamkele Mene aliipongeza Tanzania kwa kuwasilisha Hati ya kuridhia mkataba wa AfCFTA kwenye Kamisheni ya Umoja wa Afrika na kuwa nchi ya 40 kati ya nchi 55 za Afrika kufanya hivyo na alitoa wito kwa Watazania wenye vigezo stahiki kuchangamkia fursa za kazi zinazoendelea kutangazwa na Sekretarieti ya AfCFTA.

Aidha , Viongozi hao walikubaliana kuendelea kushirikiana katika masuala yanayohusu Mtangamano wa Afrika kupitia Mkataba wa AfCFTA hususani katika kukuza uwekezaji katika Sekta ya Usafirishaji na Uwezeshaji Biashara, Uongezaji thamani mazao ya kilimo na uzalishaji dawa.

Katibu Mkuu, Prof. Godius Kahyarara yupo nchini Ghana kushiriki Mkutano wa 10 wa Maafisa Waandamizi wa Biashara wa Afrika unaofanyika Accra, Ghana kuanzia tarehe 24-27 Januari 2022. Mkutano huo utafuatiwa na Mkutano wa Nane (8) wa Baraza la Mawaziri wa Biashara wa Afrika utakaofanyika kuanzia tarehe 28-29 Januari 2022.



Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mhe. Wamkele Mene, Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA).

# KAMPUNI NA WAFANYABIASHARA WA URUSI KUENDELEA KUWEKEZA TANZANIA



Naibu Katibu Mkuu - Viwanda na Biashara Dkt. Hashil Twalib Abdallah Leo tarehe 28 JanuarI, 2022 amepokea ugeni wa balozi mteule wa Tanzania nchini Urusi Mhe. Fredrick Ibrahim Kibuta.

Dkt. Hashil amemueleza fursa za Uwekezaji katika nyanja mbalimbali ambapo nchi yetu Kwa Sasa Iko tayari kupokea wawekezaji kutoka nchi ya Urusi waje wawekeze nchini Tanzania.

Aidha, Mhe. Balozi Kibuta amefurahishwa na mapokezi mazuri katika ofisi za Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara zilizoko katika Mji wa Serikali Mtumba.

Mhe. Balozi Kibuta amesema kuwa atahamikisha anashawishi makampuni na wafanyabiashara walioko Urusi kuja kuwekeza nchini Tanzania Kwa kutangaza fursa na vivutio vilivyopo nchini kwetu.

Mhe. Balozi Kibuta amesema kuwa ataimarisha mahusiano ya kibiashara baina ya Tanzania na Urusi Ili kuchochea Kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu Kama yalivyo malengo ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

# MKURUGENZI IDARA YA MAENDELEO YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA AFUNGUA MKUTANO WA KUMI WA KAMATI TENDAJI YA KUSIMAMIA MRADI WA KAIZEN ULIOFANYIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA CBE DAR ES SALAAM.




M Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Viwanda Dkt. Lugano Wilson amefungua rasmi Mkutano wa kumi wa kamati tendaji ya kusimamia mradi wa KAIZEN nchini Tanzania Leo tarehe 20 Januari, 2022 uliofanyika ukumbi wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Dar es salaam ambapo pia umeshirikisha washiriki wengine kwa njia ya mtandao kutoka makao makuu ya JICA nchini Japan.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Lugano amepongeza kwa maandalizi mazuri yaliyofanyika ya Mkutano huo uliowahusisha wabia wa maendeleo JICA nchini Tanzania na taasisi zinazoshiriki katika mradi huu zikiwemo TPSF, CTI, SIDO, CBE, EPZA, TBS, NIP, VETA na TCCIA.

Dkt. Lugano amesema kuwa Falsafa ya KAIZEN inasaidia kuongeza Tija, Ufanisi, Ubora na pia inasaidia kuongeza uzalishaji Viwandani inayopelekea kupatikana kwa fursa za ajira na kipato kwa wenye Viwanda.
"Falsafa hii ya KAIZEN imesaidia kubadilika kwa mtazamo na fikra kwa wamiliki wengi wa Viwanda inayopelekea kukua kwa biashara zao" Amesema Dkt. Lugano.

Aidha, Amesema kuwa uhamasishaji wa matumizi ya falsafa ya KAIZEN ni miongoni mwa juhudi za Wizara yetu ya kuijengea uwezo sekta ya viwanda nchini katika harakati za kutekeleza Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda
.
Dkt. Lugano amesema kuwa mpango wa serikali ni kuhakikisha sekta binafsi inashiriki kikamilifu katika kukuza uchumi wa nchi kupitia sekta ya viwanda.

Naye Mwakilishi Mkazi wa JICA nchini Tanzania ndugu Yamamura Naofumi ametoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kupitia kitengo cha KAIZEN (TKU) pia amefurahishwa na maandalizi mazuri ya mkutano huu wa Kumi wa kamati tendaji ya Mradi wa KAIZEN nchini Tanzania.
Mkutano huu umehudhuriwa na Mkuu wa Chuo cha Elimu ya biashara (CBE) Prof. Emanuel Mjema ambaye ametumia fursa hii kuwaeleza washiriki wa mkutano huo kuwa tunapaswa kuiishi Falsafa ya KAIZEN na kuhakikisha wakufunzi wanaongenezeka ili kusaidia wafanabiashara wengi zaidi nchini.
Prof. Mjema ameishukuru serikali ya Japan kwa ufadhili wa mradi huu ambao umeleta tija Viwandani kupiia falsafa hii ya KAIZEN nchini.







# WAZIRI DKT. KIJAJI AKABIDHIWA OFISI RASMI NA MWAMBE

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Ashatu K Kijaji (Mb) amekabidhiwa rasmi Ofisi na aliyekuwa Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) Mhe. Geoffrey Mwambe (Mb)

Makabidhiano hayo yalifanyika Januari 11, 2022 katika Ofisi za Wizara Mji wa Serikali Mtumba Dodoma na kushuhudiwa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara na Naibu Makatibu wakuu wa Wizara hiyo.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara yenye Muundo mpya kufuatia mabadiliko ya muundo wa Wizara na uteuzi wa Mawaziri , Naibu Mawaziri, Katibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan tarehe 08 Januari 2022 na kuwaapisha tarehe 10 Januari 2022.






# WAZIRI DKT. KIJAJI ARIPOTI WIZARANI NA KUKADHIWA OFISI RASMI




Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) ameripoti Ofisini kwake Mji wa Serikali Mtumba Dodoma mara baada ya kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan Ikulu ya Chamwino na kukabidhiwa Ofisi kutoka kwa aliyekuwa Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo

Dkt. Kijaji amepokewa na Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe aliyeambatana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara pamoja na watumishi wa wizara hiyo.

Aidha, Dkt. Kijaji amepata fursa ya kukutana na Menejimenti ya Wizara hiyo na kusisitiza kila mmoja kufanya kazi kwa bidii "Wizara yetu ni moyo wa uchumi wa Taifa letu, tukifanya vema Taifa letu litaendelea kuwa na uchumi imara zaidi".

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara yenye Muundo mpya kufuatia mabadiliko ya muundo wa Wizara na uteuzi wa Mawaziri , Naibu Mawaziri, Katibu Wakuu na Naibu Katibu Wakuu uliofanywa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan tarehe 08 Januari 2022.

# MHE. KIGAHE AIPONGEZA BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA (WRRB) KWA UTENDAJI MZURI WA MAJUKUMU YAO



Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe (Mb) akutana na menejimenti pamoja na watumishi wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) katika ofisi za Bodi zilizopo Vertinary Kilimo 1 Ghorofa ya Kwanza ambapo alitembelea ofisi (Idara zote na Vitengo) za Bodi na kusikiliza kazi na majukumu ya taasisi pamoja na changamoto walizonazo.

Katika taarifa yake Mhe. Naibu Waziri ameeleza jinsi taasisi hii ilivyoleta mageuzi ya kiuchumi mara baada ya kuanzishwa kwa Mfumo wa Stakabadhi (Warehouse Receipts System) ambao umesaidia wakulima kuondokana na changamoto mbalimbali ikiwemo changamoto ya bei, ubora wa mazao, wizi n.k

Mhe. Kigahe ameeleza kuwa licha ya uchache wa watumishi katika taasisi hii, watumishi wanapaswa kuendelea kufanya kazi kwa juhudi na kushirikiana na Taasisi nyingine zinazofanya kazi zinzoendana kwani Bodi ndio inayotegemewa na wakulima na wazalishaji wa bidhaa hasa kupitia utaratibu wa stakabadhi ghalani, mfumo ambao umeleta mapinduzi makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu.

“Ushirikiano ni muhimu kati ya Bodi, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Soko la Bidhaa na wadau wengine ambapo hii itasaidia kufanikiwa kwa mfumo na kutatua changamoto zinazojitokeza kwa sasa” Amesema Mhe. Kigahe.

Mhe. Kigahe amesema kuwa taasisi hii inapswa kuongezewa bajeti kwani ina uhitaji mkubwa katika kutekeleza majukumu ya bodi.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ndugu. Asangye Bangu ameeleza kazi mbalimbali zinazofanywa na Bodi hii ambapo amesema kwa kiasi kikubwa mfumo wa stakabadhi ghalani umesaidia kuweka bei nzuri kwa wakulima, kuanzishwa kwa mifumo ya kitaasisi imara ikiwemo Soko la Bidhaa (commodity exchange) na uimarishaji wa Ushirika, mfumo pia umesaidia kuwezesha wakulima kuwa na akaunti kwenye taasisi za fedha na malipo yote kupitia benki, Mfumo umesaidia kuondoa changamoto ya mizani, vipimo sahihi na ubora kwa kiasi kikubwa.

Aidha ameongeza kuwa bodi imejikita zaid katika matumizi ya TEHAMA ambapo imesaidia Zaidi katika utoaji wa stakabadhi kwa njia ya mtandao, Maombi ya Leseni kwa njia ya mtandao, usajili wa maghala yote nchini na sasa wanajipanga katika kuhakikisha maghala yote nchi yanafungwa mifumo ya CCTV Camera ili kuzuia wizi na kuweka usimamizi mzuri.

# WAZIRI MKUMBO AWATAKA WATUMISHI KUENDELEA KUSIMAMIA MAJUKUMU YAO



Waziri wa Viwanda na Biashara Prof. Kitila Mkumbo amewataka watumimishi wa Wizara hiyo kuendelea kusimamia majukumu yao kwa ufanisi Katika kufanikisha kusudi la Serikali huku wakitumia hekima, uaminifu na Busara.

Pia amewataka wakuu wa Idara kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki kwa watumishi kuanzia ngazi za chini kupata taarifa mbalimbali zinazoendelea ndani ya Wizara hiyo huku wakijenga Tabia ya kukutana mara kwa mara kuanzia ngazi za chini kubadilishana mawazo jambo ambalo litasaidia kuwapa wepesi kufanya kazi.

Pro. Mkumbo ameyasema hayo 7/1/2022 kwenye Hafla ya Ukaguzi wa Maendeleo ya Ujenzi wa Jengo la Wizara Mji wa Serikali Mtumba iliyoambatana na tukio la kupanda miti kwa viongozi pamoja na Watumishi wa Wizara ya Viwanda na Biashara.

**“Nichukue nafasi hii kuwashukuru watumishi wote kwa ushirikiano ambao mmetupa sisi na viongozi wenzangu kwenye Wizara maana bila nyie watumishi hakuna Chochote Cha maana.”**

"Pia tunamshukuru Rais kwa kuanzisha Ofsi hizi za Wizara hii kwani itatusaidia watumishi kukaa pamoja maana wengine wako UDOM jambo ambalo linapelekea kufanya kazi kwa mazingira tofauti" alisema .

"Sisi tunataka kuendesha furaha, lengo la maisha sio huzuni ni furaha kazini, hivyo tujitahidi kufanya kazi zetu katika mazingira ya furaha na Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kupitia ujenzi huu anatufanya kufanya kazi kwenye mazingira ya furaha ."alisema Mkumbo.

Mbali na hayo aliwataka kutambua muelekeo na Dhamira ya Serikali Chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anatamani kuona mitaa ya viwanda na kwenye biashara anataka kuona wafanyabiashara wanafanya biashara katika hali huru ili walipe kodi kwa furaha ambapo kwa mwaka jana zilizkusanywa kodi Trioni 2.5.

Nae Katibu Mkuu wa wizara hiyo Dotto James amesema kuwa wizara inatoa pongezi kwa Waziri huyo Jinsi anavyofuatilia miradi na shuguli kwa karibu .

"tunakupongeza Waziri kama Wizara Leo ni tarehe 7/1/2022 ni siku za mwanzoni mwa mwaka, tumepata Bahati ya kuongea na Sisi lakini kikubwa ni kuzungumza na watumishi na kutembelea miradi inaonyesha ni kiasi una malengo juu ya Wizara yako" amesema Dotto.

Awali akisona taarifa ya ujenzi wa jengo la ofsi ya Wizara msimamiz wa Mradi kutoka Shirika la Nyumba NHC , Leo David amesema jengo Hilo litakuwa la kisasa ambalo litakuwa na Ghorofa sita

Kuwa mpaka Sasa lipo kwenye hatua ya msingi ambayo linatazamiwa likamilike 23 oktoba mwakani kwa matumizi ya Ofsi.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara hiyo mwenyekiti wa Chama Cha wafanyakazi Thughe Josephine Mwidadi amesema kuwa wanashukuru kwa ushauri na maelekezo ya Waziri huku wakimuahidi kuyafanyia kazi kwa maslahi mapana ya Taifa .

# WAZIRI MKUMBO AONGEZA MIEZI 6 KUWASILISHA TAARIFA ZA WAMILIKI MANUFAA WA KAMPUNI




Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof.Kitila Mkumbo, ameongeza muda wa miezi sita kwa kampuni kuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).
Hata hivyo, amesema kwa kampuni zitakazoshindwa kuwasilisha hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Prof.Mkumbo ameyasema hayo leo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu kuongeza muda wa miezi sita kwa ajili ya kuwasilishwa taarifa hizo.

Amesema awali taarifa hizo zilipaswa kuwa zimewasilishwa ifikapo Desemba 31, mwaka jana lakini kutokana na maombi ya wawekezaji kuhusu kuongeza muda, hivyo serikali imeongeza miezi sita ili kutoa nafasi kwa wamiliki hao kuwasilisha taarifa zao.

Waziri huyo amesema kampuni zilizowasilisha taarifa hizo hadi jana ni 14,026 sawa asilimia 14 ya matarajio.

Amefafanua kuwa kampuni zote nchini husajiliwa na BRELA na hupaswa kutoa taarifa kadhaa ikiwamo wamiliki manufaa wa kampuni na awali hazikulazimika kisheria kutoa taarifa za waliopo nyuma ya kampuni(wamiliki manufaa) lakini kwasasa ni lazima.

“Hawa wamiliki manufaa ndio wenye mtaji na wanaendesha kampuni, hivyo Benki ya Dunia na taasisi zingine kimataifa zimehimiza kueleza kwa uwazi umiliki wa kampuni,”amesema.

Amesema kutokana na umuhimu wa taarifa hizo na kwa mamlaka aliyonayo kisheria ameongeza muda huo hadi Juni 30, mwaka huu ili wamiliki wote watimize matakwa ya sheria.

"Niwahimize wamiliki wote watumie muda vizuri wa nyongeza na sheria ipo wazi kwa yule ambaye hatawasilisha taarifa zake hatua gani zitachukuliwa dhidi yake,katika kujenga mahusiano mema na wafanyabiashara tumekubaliana kuongeza muda huu,"amesema.
Naye, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Makampuni na Majina ya biashara kutoka BRELA,Meinrad Rweyamamu, amesema sheria ya makampuni imeweka utaratibu pale ambapo mtu atachelewesha kuwasilisha taarifa atakumbana na adhabu ya kulipa Sh.2500 kila mwezi.

"Kwa kila mwezi ambao atakuwa amechelewesha taarifa atapaswa kulipa kiasi hicho, sambamba na hilo ikibainika haikuwasilisha taarifa za wamiliki manufaa au kuwasilisha taarifa ambazo si za kweli Mahakama itaipiga adhabu kampuni hiyo ya faini kuanzia Sh.Milioni tano hadi 10,"amesema.

Amesema kampuni ambazo zimekuwa zikipeleka taarifa za mwaka ni zaidi ya 140,000 na kwamba bado kampuni nyingi hazipeleki taarifa zao BRELA hivyo wanatarajia kutoa taarifa ya kampuni zisizo hai ili zihuishe taarifa zao







Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Mhe. Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) kuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara leo tarehe 10 Januari, 2022 Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Mhe. ExaudKigahe(Mb) kuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara leo tarehe 10 Januari, 2022 Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akimuapisha Bw. Ally S. Gugu kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara (Uwekezaji) leo tarehe 10 Januari, 2022 katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino Mkoani Dodoma.



# WAZIRI DKT. KIJAJI AKABIDHI OFISI RASMI KWA NAPE

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) akabidhi Ofisi yake ya awali kwa Waziri wa Mpya wa Habari, Mawasiliano na Teknologia ya Habari, Mhe. Nape Moses Mnauye (Mb)

Makabidhiano hayo yanafuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri ambayo yalifanywa na Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan siku ya Jumamosi na kuapishwa Januari 10, 2022 kwa kumteua Mhe. Nape Moses Mnauye (Mb) kuwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknologia ya Habari na kumuamisha Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb) kuwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

Hafla hiyo fupi imefanyika katika Ofisi ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknologia ya Habari Mji wa Serikali Mtumba Dodoma, Leo Januari 11, 2021







# MHE. KIGAHE AWATAKA WAJASIRIAMALI WANAOFANYA BIASHARA KATIKA MAENEO YOTE YA SIDO NCHINI AMBAO WANADAIWA KODI WALIPE MARA MOJA FEDHA WANAZODAIWA KABLA HAWAJACHUKULIWA HATUA KALI ZA KISHERIA

Naibu Waziri Wizara ya Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe (Mb) Ameyasema hayo leo alipotembelea ofisi za SIDO Mkoa wa Dar es salaa zilizopo Vingunguti na kujionea shughuli mbalimbali za uzalishaji zinazofanywa na Wajasiliamali waliopo katika eneo moja linalosimamiwa na SIDO.

Mhe. Kigahe amesema kuwa shughuli za ujasiliaamali ndio zinasaidia ajira kwa wingi nchini hivyo SIDO ina jukumu kubwa la kuhakikisha wanawasaidia Wajasiliamali wadogo hasa mpango wa viatamizi (incubation) ambapo wale ambao wamekuwa zaidi wanatoka na kutoa nafasi kwa wengine.

Ameongeza kwa kusema kuwa faida ya wajasiriamali kuzalisha katika eneo linalosimamiwa na SIDO ina faida kubwa kubwa kusaidia wajasiliamali kuzalisha kwa gharama ndogo, kupata usaidizi wa karibu katika teknolojia na mafunzo mbalimbali, miundombinuwezeshi kama majengo na kushirikiana na wajasiliamali wengine waliopo katika eneo moja.

Mhe. Kigahe ameagiza wajasiriamali wote wanaodaiwa kodi ya pango katika majengo ya SIDO kote nchini kuhakikisha wanalipa madeni yao wanayodaiwa na SIDO ili kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kufanyia biashara katika maeneo mengine ili kusaidia Wajasiriamali wengi zaidi kupata majengo ya kufanyia shughuli zao.



Naye meneja wa SIDO Mkoa wa Dar es salaam ndugu Ridhiwani Matange amemshukuru sana Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuwatembelea kwani ni fursa nzuri ya kueleza changamoto wanazokutana nazo ili aweze kuzifikisha katika ngazi za juu.
Bwana Matange ameongeza kwa kueleza changamoto ya bajeti ambapo amesema SIDO haifanyi biashara na inatoa huduma hivyo ni vyema wakaongezewa fedha ambazo zitasaidia shughuli wanazofanya ikiwemo ukarabati wa majengo na ujenzi wa majengo mapya nay a kisasa kwa ajili ya Wajasiriamali wengi zaidi.
Ameongeza kwa kusema pia changamoto nyingine wanayokutana nayo ni kwa Wafanyabiashara wasio waaminifu wamekuwa hawalipi kodi na kulimbikiza madeni makubwa na kudhoofisha utendaji wa SIDO katika Mkoa wa Dar es salaam na maeneo mengine.
Aidha Mkurugenzi wa kiwanda cha "Star Natural Products" kilichopo katika eneo la SIDO Bwana George amefurahi sana kwa ujio wa Mhe. Naibu Waziri na Mkurugenzi Mkuu wa SIDO

Mhandisi Prof. Sylivester Mpanduji kwani kuja kwao kunawapa faraja ya kuona serikali ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan imekuwa ikiwajali sana wajasiriamali nchini kwani wamekuwa wakipatiwa mikopo isiyokuwa na vikwazo na kwa kujenga majengo yenye gharama nafuu kwa Wajasiriamali kufanya shughuli zao.
da na Biashara kupitia kitengo cha KAIZEN (TKU) pia amefurahishwa na maandalizi mazuri ya mkutano huu wa Kumi wa kamati tendaji ya Mradi wa KAIZEN nchini Tanzania.
Mkutano huu umehudhuriwa na Mkuu wa Chuo cha Elimu ya biashara (CBE) Prof. Emanuel Mjema ambaye ametumia fursa hii kuwaeleza washiriki wa mkutano huo kuwa tunapaswa kuiishi Falsafa ya KAIZEN na kuhakikisha wakufunzi wanaongenezeka ili kusaidia wafanabiashara wengi zaidi nchini.
Prof. Mjema ameishukuru serikali ya Japan kwa ufadhili wa mradi huu ambao umeleta tija Viwandani kupiia falsafa hii ya KAIZEN nchini.

# TANZANIA NA MISRI ZAKUBALIANA USHIRIKIANO KATIKA KUIMARISHA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA KILIMO, USAFIRI, MIUNDOMBINU YA UMEME, MAJI NA USAFIRI

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji amekutana na balozi wa Misri nchini Tanzania Mhe. balozi Mohamed Gaber Abulwafa na kujadiliana masuala mbalimbali ya Uwekezaji na fursa mbalimbali zilizopo baina ya nchi hizi mbili.

Mhe. Dkt. Kijaji amesema kuwa uhusiano na ushirikiano wa Uwekezaji baina ya Misri na Tanzania umekuwa ukiimarika zaidi baada ya ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyoifanya tarehe 10 Novemba, 2021 kukutana na Rais wa Misri Mhe. Abdel Fattah Al Sisi.

Mhe. Dkt. Kijaji ameeleza kuwa fursa za biashara na uwekezaji kati ya Misri na Tanzania ambapo kwa hivi sasa biashara baina ya nchi hizo mbili imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 84.3 mwaka 2018 hadi kufikia Shilingi Bilioni 87.3 mwaka 2020 hivyo kuna kila sababu yakuendeleza majadiliano na makongamano ya biashara baina ya nchi hizi mbili ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara kutumia fursa za uwekezaji.



Naye balozi wa Misri nchini Tanzania Mhe. Balozi Mohamed Gaber Abulwafa amesema kuwa Nchi ya Misri imewekeza nchini Tanzania katika miradi 26 yenye thamani ya kiasi cha Shilingi Trilioni 3.1 na kutengeneza ajira 2,206 kwa watanzania.

Mhe. Balozi Mohamed Gaber Abulwafa amesema kuwa wawekezaji kutoka Misri walishafika nchini Tanzania katika Kongamano la Biashara lililofanyika nchini Tanzania ambapo wafanyabiashara wa Misri walipata fursa mbalimbali za kuwekeza na sasa wanaendelea na taratibu mbalimbali kuja kuwekeza Tanzania katika sekta ya Kilimo na Mifugo hasa biashara ya korosho, parachichi na Mahindi.

Aidha ameongeza kuwa Misri wapo katika hatua za ukamilishwaji wa kuanza kwa usafiri wa abiria kwa njia maji marine transport kutoka Misri hadi Tanzania ili kukuza Uwekzaji na Biashara na kurahisha usafirisjhaji wa bidhaa katika nchi hizi mbili.

Mhe. Dkt. Kijaji amemalizia kwa kusema kuwa Nchi ya Misri imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati katika nchi ya Tanzania ukiwemo ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere (JNHPP-MW2115) unaotarajiwa kukamilika Mwezi Juni 2022 na kusaidia Viwanda vyetu kuzalisha kwa uhakika kwani changamoto ya umeme nchini itakuwa imekwisha.


06:23
Back
Expo 2020 Business App
182
DAYS OF BUSINESS PROGRAMMING
Start Networking
My Agenda
Expo Participants
District 2020
App ya Expo 2020 Business
Inakurahisisishia kupata taarifa zaidi
kuhusu maonesho ya EXPO 2020 DUBAI
Panga mikutano ya Kibiashara (B2B)
Jua namna ya kushiriki
DOWNLOAD
Available on the App Store
Google play



Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Viwanda na Biashara
S.L.P 2996, 40478 Dodoma,Tanzania Mji wa
Serikali Mtumba, Mtaa wa Viwanda
Telephone: +255 26 2963470
Nukushi: +255 26 2963117
Barua pepe: ps@mit.go.tz gcu@mit.go.tz
www.mit.go.tz